## Alishuhudia unyama mkubwa akiwasaidia manusura

# ALINUSURIKA KIFO KATIKA MAUAJI YA RWANDA



**Bi Susanne Brezina akielezea masaibu yaliyomkumba akiwa nchini Rwanda wakati wa mauaji ya halaiki wakati wa makumbusho. Kushoto ni rais wa Rwanda Paul Kagame.** *Picha/MAKTABA*

Ni miaka kumi na mitano tangu mauaji ya halaiki kufanyika nchini Rwanda na inakadiriwa ya kuwa takribani watu milioni mbili waliuawa kitakili baada ya vita ya wenyewe kwa wenyewe kuzuka kati ya Wahutu na Watutsi.

Kwa wahasiriwa na hata wale walioshuhudia mauaji hayo bado ni kumbukumbu ambayo inaleta majuto na huzuni si haba.

Na RACHUONYO DUNCAN

Ni wazi ya kuwa itawachukua muda mrefu kusahau yale yote yaliyofanyika mwaka wa 1994 kwani licha ya idadi kubwa kupoteza maisha, wengi walibaki kuwa yatima na hata wengine kukosa kuwaona wapendwa wao hadi leo.

Bi Susanne Brezina mwenye umri wa miaka 43, bado hajasahau mauaji ya ukatili aliyoshuhudia dhidi ya jamii mbili za Hutu na Tutsi.

Licha ya hayo, alijipata tena katika msukosuko hapa nchini Kenya wakati wa ghasia baada ya uchaguzi mkuu wa 2007.



Bi Brezina ambaye ni raia wa Austria na kifungua mimba katika familia ya watoto watatu alifanya wengi kudodokwa na machozi alipokuwa akieleza masaibu yake wakati wa makumbusho ya mamilioni ya raia waliouawa katika mauaji ya halaiki nchini Rwanda mwaka wa 1994.

Mauaji ya kikatili

Kulingana naye, alisema ya kuwa mwaka wa 1994 alikuwa na umri wa miaka 28 wakati mauaji ya kikatili yalikuwa yanaendelea.

Bi Brezina ambaye alikuwa mhudumu wa kujitolea alisema wakati huo mji mkuu wa Kigali ulikuwa haupitiki kamwe kwani waasi walikuwa wameteka nyara nchi nzima.

"Nilikuwa mzungu pekee yangu na ilikuwa na shida ya kusaidia wengi wa raia walikuwa na majeraha, sikuweza kuamini macho yangu," asema.

Alisema ya kuwa alikuwa anapita miili ya watu ambao walikuwa wametapakaa kila sehemu. "Mji wa Kigali ulikuwa haupitiki na waasi walikuwa tayari wamepora kila kitu na hata kubomoa baadhi ya majengo katika mji huo.

Bi Brezina anasema ya kuwa alikutana na umati mkubwa wa watu ambao wengi wao walikuwa watoto na akina mama ambao walikuwa wanatorokea nchi jirani kama vile Burundi na Uganda.

"Hata mimi ilikuwa na uoga si haba, lakini sikuwa na shida na waasi kwani walikuwa tu hawataki kuona mtu kutoka kabila la Watutsi," asema.

Alisema kuwa bado itamchukua miaka mingi sana kusahau yale yote aliyoshuhudia nchini Rwanda na hapa nchini.

"Sijui kama nitasahau, la msingi ni kuandika kitabu ambacho kitawafundisha jamii ya Afrika," aeleza.

Fauka ya hayo, anazidi kueleza ya kuwa alishangazwa sana kuona mauaji ya kikatili nchini Kenya baada ya uchaguzi mkuu mwaka wa 2007. "Matokeo ya vita huwa ni ya uchungu na sioni ni kwa nini watu wanatamani Vita. Sipendi kamwe kutaka kushuhudia maafa kama nilivyoona nchini Rwanda na Kenya," aliambia Taifa Leo.

i Brezina anasema ya kuwa ilimbidi kuwaficha wazazi wake ambao walikuwa na hamu na ghamu kujua hali yake.

"Nilipokuwa nikiondoka, niliwaambia ya kuwa ninaenda nchi ya Burundi lakini nikaamua kwenda Kigali, Rwanda wakati vita ilipozuka nikiwa humo," asema.

Licha ya hayo, anasema ya kuwa wakati huo wengi wa raia walikuwa na shida hata ya mawasiliano.

Baada ya siku mia za vita dhidi vya kikabila, wageni kutoka Umoja wa Mataifa walianza kuingia na hapo ndipo alipojiunga nao na hata kuanza kuwasiliana na wazazi.

### WALISHANGAA KUNIONA HAI

"Nilipowaambia ya kuwa nilikuwa nchini Rwanda, kila mmoja alikuwa na wasiwasi lakini niliamua kubaki kusaidia wahasiriwa wa machafuko hayo," aeleza kwa jasiri.

Hata baada ya kusafiri Austria, wengi hawakuamini kumwona akiwa bila ya majeraha mwili kwani habari zilienezwa duniani kote ya kuwa nchi ya Rwanda imegeuka na kuwa nchi ya mauaji ya halaiki.

"Kila mtu alishangazwa na jinsi nilivyoponea chupuchupu nchini Rwanda, ni Mungu tu aliyeweza kuniokoa," asema Bi Brezina.

Kuzuka kwa kipindupindu

Bi Brezina mwenye miaka 43, alisema ya kuwa takribani watu milioni moja walikuwa tayari walikuwa wanataka kuvuka kuelekea DRC Congo wakati kila mmoja aliamua kukata kiu na maji kutoka Ziwa Kivu.

> **'Ataandika kitabu kuhusu jinsi alivyoona miili ya watu imetapakaa kila mahali'**

Baada ya siku chache, watu nusu milioni walikuwa wanaugua kipindipindu na hapo ndipo walianza kuaga dunia.

"Huwezi kuamini, wengi wao walikufa na kila mtu alikuwa anaogopa hata kunywa chochote," asema kifungua mimba.

Kulingana na mwanadada huyo, alikuwa jasiri wa kupindukia kwani alikumbana na ukatili ambao hadi wa leo ni kumbukumbu maishani mwake.

"Baadhi ya majengo yalikuwa yamebomolewa na hata kupata chakula ilikuwa shida sana, jamii ya Wahutu walikuwa hawataki kuona jamii ya Watutsi. Ilikuwa chuki kubwa mno," asema.

Alisema idadi kubwa ya watu walikufa kutokana na kuzuka kwa kipindupindu.

Zaidi ya hayo, Bi Susanne Brezina anasema ya kuwa ilikuwa kama ndoto kwake na baada ya muda mrefu alikuwa hawezi kamwe kuamini yale yote alikuwa anashuhudia nchini Rwanda.

"Nilikuwa nikipata na watu ambao walikuwa wanataka msaada kwangu lakini sikuwa na la kufanya," asema.

Licha ya hayo, aliambia Taifa Leo ya kuwa angeweza hata kutoka nchini humo kwani usafiri kila mahali ulikuwa umetatizwa pakubwa na hakuna yeyote aliyekumbaliwa kutumia uwanja wa ndege.

### HIMIZO

Balozi wa Rwanda humu nchini George William Kayonga alihimiza nchi za Afrika kutokubali wachochezi wanaogawanya jamii kutokana na siasa duni.

"Ni jambo la kushangaza ni kuona watu wa nchi moja wakipigana wenyewe kwa wenyewe, hatutaki kuona tena nchi yoyote hapa Afrika katika hali kama ilivyokuwa nchini Rwanda," asema balozi.

Balozi huyo alisema ya kuwa Kenya ni nchi ambayo inasifika duniani si haba na haitakuwa vyema kuona tena watu wakigawanywa kutokana na kabila lao.

Balozi Kayonga aliwahimiza jamii ya Rwanda kutokubali tena mauaji kufanyika na aliwaahidi waasiriwa wa mauaji ya halaiki ya kuwa Serikali ya Rwanda itafanya juu chini kuhakikisha ya kuwa kila moja amepata msaada.

Balozi huyo aliwahimiza sana Wakenya kutokubali kugawanywa kutokana na siasa wala kabila. "Hatutaki kuona tena machafuko kama yalivyokuwa baada ya uchaguzi wa Decemba 2007. Sio vyema hata kidogo," asema Balozi Kayonga.

Licha ya hayo, alisema ya kuwa matokeo ya vita huwa ni pigo kubwa sana kwa nchi kwani huchukua muda mrefu kwa nchi kuendelea kiuchumi.

"Nchi ya Rwanda ilikuwa imepiga hatua muafaka kimaendeleo, lakini baada ya mauaji ya halaiki kufanyika mwaka wa 1994, nchi yetu ilirudi nyuma sana," asema.

Isitoshe, alisema kuwa matokeo ya Rwanda yanafaa kuwa funzo kwa nchi za Afrika kwa jumla.

"Tunataka amani katika nchi za Afrika, kama mataifa yote yalishuhudia matokeo ya Rwanda, nina imani hakuna yeyote ambaye angetaka tena kuchochea wengine kupigana," asema.



**BALOZI wa Rwanda nchini Kenya George Williams Kayonga mwenye suti ya milia na wanawe Jasmine(katikaiti) na Alvine kushoto wakiwa katika makumbusho ya mauaji ya halaiki nchini Rwanda katika ukumbi wa Serena jijini Nairobi.** *PICHA/D.RACHUONYO*